

TANGAZO LA SERIKALI Na. 494 la tarehe 21/7/2023

SHERIA YA KAMPUNI,
(SURA YA 212)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 483(2))

KANUNI ZA KAMPUNI ZA UMILIKI MANUFAA ZA MWAKA 2023

MPANGILIO WA KANUNI

Kanuni Maelezo

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
TAARIFA ZA WAMILIKI MANUFAA

3. Taarifa za wamiliki manufaa.
4. Tamko la maslahi ya manufaa.
5. Mabadiliko ya wamiliki manufaa.
6. Zuo la utoaji taarifa za wamiliki manufaa.

SEHEMU YA TATU
REJESTA YA WAMILIKI MANUFAA

7. Rejesta ya wamiliki manufaa.
8. Kukataliwa usajili.
9. Uwasilishaji wa nyaraka.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

10. Makosa na adhabu.
11. Usiri wa taarifa.
12. Kuongeza muda.
13. Kufutwa kwa Kanuni.

SHERIA YA KAMPUNI,
(SURA YA 212)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 483(2))

KANUNI ZA KAMPUNI (UMILIKI MANUFAA) ZA MWAKA 2023

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zinajulikana kama Kanuni za Kampuni (Umiliki Manufaa) za mwaka 2023.

Tafsiri
Sura ya 212

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitajika vinginevyo-
“Sheria” maana yake ni Sheria ya Kampuni;
“maslahi ya manufaa” maana yake ni maslahi makubwa ya kiuchumi au faida au uwezo mkubwa wa kufanya maamuzi katika kampuni;
“mmiliki manufaa” itakuwa na maana kama ilivyoainishwa kwenye Sheria;
“mmiliki manufaa halisi” maana yake ni mtu asilia mwenye kumiliki au anayemiliki maslahi ya manufaa katika kampuni na jina lake kusajiliwa katika rejesta ya wamiliki wa kampuni;
“mmiliki manufaa asiye halisi” maana yake ni mtu asilia mwenye kumiliki au atakayemiliki maslahi ya manufaa katika kampuni ambaye hajasajiliwa katika rejesta ya wamiliki wa kampuni;
“umiliki wa moja kwa moja” maana yake ni umiliki manufaa halisi;
“umiliki usio wa moja kwa moja” maana yake ni umiliki manufaa usio halisi;
“mmiliki aliyesajiliwa” maana yake ni mtu yeyote ambaye majina yake yameorodheshwa katika rejesta ya

wamiliki wa kampuni;
“Msajili” maana yake ni Msajili wa Kampuni aliyeteuliwa
chini ya kifungu cha 450 cha Sheria.

SEHEMU PILI
TAARIFA ZA WAMILIKI MANUFAA

Taarifa za
mmiliki
manufaa

3.-(1) Kampuni iliyoanzishwa chini ya Sheria
itawasilisha kwa Msajili taarifa za wamiliki manufaa
wake.

(2) Kampuni itahakikisha inachukua hatua stahiki
za kutambua wamiliki manufaa wake na kuingiza taarifa
zao katika rejesta yake ya wamiliki manufaa kama
ilivyoelekezwa katika kifungu cha 14(2)(b) cha Sheria.

T.S. Na.
41 la 2005

(3) Kampuni yenye mmiliki manufaa halisi
itawasilisha kwa Msajili taarifa za mmiliki manufaa kwa
kuzingatia utaratibu ulioelekezwa kwenye mfumo wa
upokeaji wa taarifa za umiliki manufaa ndani ya siku
thelathini kuanzia tarehe ambayo jina lake limeingizwa
kwenye rejesta ya wamiliki na wamiliki manufaa.

T.S Na
126 la 2014

(4) Kampuni yenye mmiliki manufaa asiye halisi
itawasilisha kwa Msajili taarifa za mmiliki manufaa huyo
kwa kujaza Fomu Na. 14b iliyoainishwa kwenye Kanuni
za Fomu za Kampuni ndani ya siku thelathini kuanzia
tarehe ambayo jina lake limeingizwa kwenye rejesta ya
wamiliki na wamiliki manufaa.

(5) Pale ambapo mmiliki manufaa asiye halisi
anapokoma kuwa mmiliki manufaa, kampuni itatakiwa,
baada ya kulipa ada kama zilivyobainishwa kwenye
Kanuni za Ada, kuwasilisha notisi kwa Msajili kuhusu
mabadiliko hayo kwa kujaza Fomu Na. 14c iliyoainishwa
kwenye Kanuni za Fomu za Kampuni ndani ya siku
thelathini kuanzia tarehe ya kukoma kuwa mmiliki
manufaa.

(6) Kampuni itakayoshindwa kuwasilisha fomu
ndani ya muda uliobainishwa itawajibika kulipa ada ya
ucheleweshaji kwa Msajili kama ilivyoainishwa kwenye
Kanuni za Ada.

Tamko la
maslahi ya
manufaa.

T.S. Na.
41 la mwaka
2005

T.S. Na.
41 la mwaka
2005

T.S Na.
126 la 2014

Mabadiliko ya
wamiliki
manufaa
T.S Na.

4.-(1) Mtu ambaye jina lake limeingizwa katika rejesta ya wamiliki na wamiliki manufaa wa kampuni kama mmiliki wa hisa wa kampuni hiyo lakini si mmiliki halisi wa manufaa, atawasilisha kwenye kampuni tamko kuhusu umiliki halisi wa manufaa kwa kujaza Fomu Na. 14d iliyoainishwa kwenye Kanuni za Fomu za Kampuni ndani ya muda wa siku thelathini kuanzia tarehe ambayo jina lake limeingizwa kwenye rejesta ya wamiliki na wamiliki manufaa:

Isipokuwa kwamba, pale ambapo kuna mabadiliko kuhusu maslahi ya manufaa, mmiliki aliyesajiliwa katika rejesta ya wamiliki wa kampuni ambaye si mmiliki halisi wa manufaa, atalazimika ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya mabadiliko, kutoa tamko kuhusu mabadiliko hayo kwenye kampuni kwa kujaza Fomu Na. 14d iliyoainishwa kwenye Kanuni za Fomu za Kampuni.

(2) Mmiliki manufaa asiye halisi atawasilisha kwenye kampuni tamko litakalobainisha maslahi aliyonayo kwa kujaza Fomu Na. 14e iliyoainishwa kwenye Kanuni za Fomu za Kampuni ndani ya muda wa siku thelathini kuanzia tarehe ya kupata maslahi ya manufaa katika kampuni:

Isipokuwa kwamba, pale ambapo kuna mabadiliko kuhusu maslahi ya manufaa, mmiliki manufaa atalazimika ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya mabadiliko, kutoa tamko kuhusu mabadiliko hayo kwenye kampuni kwa kujaza Fomu Na. 14e iliyoainishwa kwenye Kanuni za Fomu za Kampuni.

(3) Pale ambapo tamko chini ya kanuni hii limepokelewa na kampuni, kampuni itaingiza taarifa za tamko hilo kwenye rejesta ya wamiliki na wamiliki manufaa wa kampuni, na baada ya kulipa ada kama zilivyobainishwa kwenye Kanuni za Ada zinazolipwa kwa Msajili, itawasilisha kwa Msajili taarifa hizo kwa kujaza Fomu Na. 14b ndani ya muda wa siku thelathini baaada ya kupokea tamko hilo.

5.-(1) Kampuni itatakiwa, baada ya kulipa ada kama zilivyoainishwa kwenye Kanuni za Ada zinazolipwa kwa Msajili, kuwasilisha kwa Msajili taarifa za

126 la 2014
T.S Na.
41 la 2005

mabadiliko ya mmiliki manufaa asiye halisi kupitia Fomu Na. 14f iliyoainishwa kwenye Kanuni za Fomu za Kampuni ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya mabadiliko.

(2) Endapo kutatokea hamisho la hisa au ongezeko au punguzo la mtaji wa kampuni au badiliko la muundo wa mtaji wa hisa za kampuni au mabadiliko ya haki za kupiga kura yatakayosababisha mabadiliko ya maslahi ya manufaa, kampuni pamoja na taratibu zilizowekwa kwenye Sheria, itawasilisha kwa Msajili notisi kupitia Fomu Na. 14f iliyoainishwa kwenye Kanuni za Fomu za Kampuni ikionesha mabadiliko ya umiliki manufaa katika kampuni.

T.S Na.
41 la 2005

(3) Msajili hatasajili notisi ya upatikanaji wa hisa au nyaraka yoyote inayohusu mabadiliko ya hisa zilizogawiwa au haki ya kupiga kura hadi pale matakwa ya kanuni ndogo ya (2) yatakapokuwa yametekelezwa.

(4) Notisi ya mabadiliko ya umiliki manufaa iliyorejewa katika kanuni hii itasainiwa na angalau mkurugenzi mmoja wa kampuni au katibu wa kampuni na nakala halisi iliyohibitishwa ya nyaraka rasmi ya utambulisho wa kila mmiliki manufaa itawasilishwa kwa Msajili.

Kutokutoa
taarifa za
wamiliki
manufaa.

6. Kampuni haitatumia au kutoa taarifa yoyote kuhusu mmiliki manufaa wake isipokuwa kwa ajili ya-

- (a) mawasiliano na mmiliki manufaa husika;
- (b) kutekeleza matakwa ya Sheria;
- (c) kutekeleza amri ya mahakama;
- (d) kutekeleza maelekezo ya mmiliki manufaa husika; au
- (e) kutekeleza matakwa ya sheria nyingine yoyote.

SEHEMU TATU

REJESTA YA WAMILIKI MANUFAA

Rejesta ya
wamiliki
manufaa

7.-(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 451A cha Sheria, taarifa za wamiliki manufaa wa kila kampuni zilizowasilishwa kwa Msajili kwa mujibu wa Kanuni hizi zitaingizwa na kutunzwa na Msajili kwenye rejesta ya wamiliki manufaa.

(2) Taarifa za wamiliki manufaa wa kampuni zitakazotunzwa na Msajili kwenye rejesta ya wamiliki manufaa zitatolewa kwa mamlaka idhinishwa zilizoainishwa katika kifungu cha 451B cha Sheria baada ya maombi ya maandishi kuwasilishwa kwa Msajili.

Kukataliwa
usajili

8.-(1) Msajili anaweza kukataa kusajili nyaraka yoyote ya kampuni inayopaswa kusajiliwa chini ya Sheria ikiwa-

- (a) taarifa za mmiliki manufaa hazikuwasilishwa; au
- (b) hakuridhika kwamba kampuni imewasilisha taarifa sahihi na za wakati kuhusu wamiliki manufaa wa kampuni.

(2) Endapo Msajili atakataa kusajili nyaraka kwa mujibu wa kanuni hii, atapaswa kuwajulisha wahusika ipasavyo kuhusu uamuzi huo.

Uwasilishaji wa
nyaraka

9. Nyaraka yoyote inayopaswa kuwasilishwa kwa Msajili chini ya Kanuni hizi inaweza kuwasilishwa katika muundo na kwa utaratibu utakaojumuisha muundo wa kielektroniki na mawasiliano kwa njia ya kielektroniki kama Msajili atakavyoona inafaa.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

Makosa na
adhabu

10. Mtu ambaye-

- (a) atashindwa kutunza kumbukumbu za wamiliki manufaa;
- (b) atashindwa kuwasilisha kwa Msajili taarifa kuhusu mabadiliko ya umiliki manufaa wa kampuni;
- (c) atashindwa kuwasilisha kwa Msajili tamko lenye taarifa za wamiliki manufaa wa kampuni; au

(d) atakiuka masharti yoyote ya Kanuni hizi, atakuwa ametenda kosa na endapo akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi shilingi milioni kumi.

Kutokutoa
taarifa za siri

11. Msajili, afisa aliyeidhinishwa, mamlaka au

vitengo vilivyoainishwa chini ya kifungu cha 451B cha Sheria hawataruhusiwa, hata baada ya ukomo wa ajira zao, kuweka wazi au kutoa taarifa za siri zilizopatikana kwa mujibu wa Kanuni hizi kwa mtu yeyote ambaye hajaidhinishwa.

Nyongeza ya muda

12.-(1) Endapo muda wa kuwasilisha taarifa umeainishwa katika Kanuni hizi na endapo kampuni imeshindwa kuwasilisha taarifa hizo ndani ya muda ulioainishwa, kampuni hiyo inaweza kuwasilisha kwa Msajili maombi ya nyongeza ya muda kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hizo.

(2) Baada ya kujiridhisha na sababu zilizotolewa, Msajili anaweza kuongeza muda wa kuwasilisha nyaraka kwa kipindi kisichozidi siku thelethini.

Kufutwa kwa kanuni
TS. Na. 391 la
2021

13. Kanuni za Kampuni (Umiliki Manufaa) za mwaka 2021 zinafutwa.

Dodoma,
23rd June, 2023

ASHATU K. KIJAJI,
Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na
Biashara